



**MUONGOZO WA UGAWAJI WA KITAMBULISHO CHA MJASIRIAMALI
(SEKTA ISIYO RASMI)**

Kama ilivyoelekezwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kikao kazi kati ya TRA, Wakuu wa Mkoa na Makatibu Tawala naleta kwenu muongozo huu kwa ajili ya kuratibu zoezi la ugawaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo wadogo (Machinga) kama ifuatavyo:-

1. Awe na Mauzo ghafi yasiyozidi Shilingi Milioni Nne (Tshs.4,000,000/=) kwa mwaka.
2. Awe hawajahi kusajiliwa na TRA na kupewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) isipokuwa wale waliokwisha sajiliwa awali na kupata kitambulisho au kama Mlipakodi.
3. Anatakiwa ajaze fomu maalumu inayopatikana kwa Mkuu wa Mkoa kama mfanyabiashara wa Sekta isiyo rasmi (mfano. Mama/Baba Lishe, Mmachinga n.k) mfano wa fomu umeambatishwa.
4. Mjasiriamali atalipa Shilingi elfu ishirini (Tshs.20,000/=) kwa Mkuu wa Mkoa. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itaziweka pesa zote ilizokusanya kwenye akaunti ya Kamishna wa Kodi za Ndani kwenye benki zilizoidhinishwa kukusanya Mapato. Fedha hizi zitalipwa kupitia mfumo wa malipo ujulikanao kama Revenue Gateway System (RGS) kupitia TIN ya Katibu Tawala wa Mkoa husika. Wakati wa usajili wa malipo kwenye RGS mlipaji atatumia GFS code 11111104. Baada ya malipo atapata risiti ya mtandao kwa malipo yote aliyowasilisha.

ANGALIZO

Atakayefanya udanganyifu ili kupata kitambulisho atachukuliwa hatua stahiki kupitia ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa kitambulisho hicho.

"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

Charles E. Kichere
KAMISHNA MKUU